



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

MKOA WA KILIMANJARO

Simu Na.2758367

Fax No. 2758367

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 176

MWANGA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.

15/12/2022

TANGAZO LA MAFUNDI WA KUJENGA MAJENGO MATANO KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA MWANGA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga amepokea Fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa majengo matano katika Hospitali ya Wilaya ya Mwanga

Majengo yatakayo jengwa ni kama yanavyoonekakana hapa chini:-

- 1.Jengo la mama na motto zabuni namba LGA/048/HQ/2022/2023/NC/03
- 2.Wodi ya wanaume na wanawake zabuni namba LGA/048/HQ/2022/NC/04
- 3.Jengo la kuhifadhi maiti Zabuni namba LGA/048/HQ/2022/2023/NC/05
- 4.Jengo la Kufuria Zabuni namba LGA/048/HQ/2022/2023/NC/06
- 5.Kichomeo taka Zabuni namba LGA/048/HQ/2022/2023/NC/07

Hivyo basi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga anapenda kuwatangazia mafundi wote (Local Fundi) na Tasisi za Serikali wenye uwezo wa kujenga majengo ya Serikali waweze kutuma maombi kwa ajili ya ujenzi wa majengo tajwa hapo juu.

Kablasha la zabuni kwa ajili ya kujaza gharama za ujenzi na mahitaji mengine litapatikana katika ofisi ya Usimamizi wa manunu (w)

Sifa mwombaji:-

1. Awe raia wa Tanzania mwenye uelewa mzuri wa lugha ya Kiswahili / Kingereza
 2. Awe na umri wa miaka 18 na kuendelea.
 3. Awe na timu ya kutosha ya mafundi wa fani mbalimbali za ujenzi na awe na uwezo wa kuwasimamia kazi.
 4. Awe na uwezo wa kuandaa mpango kazi na kutekeleza mpango kazi wa mradi na kumaliza kazi iliyopangwa kwa wakati uliokusudiwa.
 5. Awe mwadilifu na mwaminifu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake ya kiufundi.
6. Awe na zana zote za kazi.
7. Awe tayari kusikiliza na kupokea maelezo yote ya watalaam

Uzoefu:-

1. Uzoefu wa kuanzia miaka mitano(5) na kuendelea katika kazi ya ujenzi..
2. Awe amefanya kazi yoyote ya ujenzi au ukarabati wa majengo ya Serikali walau miradi mitatu na hati ya huduma(certificate of Service/payment) au mikataba ya miradi alioitekeleza kwa uthibitisho.(ambatanisha uthibitisho)
3. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri ramani/michoro mbalimbali ya ujenzi kwa lugha ya kiufundi.

Maombi yote yawekwe katika bahasha iliyofungwa vizuri na ndani ya bahasha hiyo utaweka nakala mbili za kablasha la zabuni na Halisi moja (original) na kuandika juu ya bahasha anuani ifuatayo:- **Katibu wa Bodi ya Zabuni (w) S.L.P 176, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga**, mwisho wa kupokea maombi hayo ni saa 4:00 asubuhi siku ya jumatano tarehe 28/12/2022 na ndio siku ya ufunguzi.

Sehemu ya kuwasilisha maombi hayo ni ofisi ya Kitengo cha manunuzi Halmashauri ya Wilaya ya mwanga utatumbukiza katika tender box.

Ufunguzi wa maombi hayo utafanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga mbele ya waombaji watakaopendelea kuhudhuria ufunguzi huo.

Tangazo limetolewa Na,



Mwajuma A. Nasombe

**MKURUGENZI MTENDAJI (H/W)
MWANGA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
YA MWANGA**